

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



BUNGE LA TANZANIA

**HOTUBA YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU AZIMIO LA
KURIDHIA MKATABA WA KIMATAIFA WA KUZUIA UENDELEZAJI,
UZALISHAJI, ULIMBIKIZAJI WA SILAHA ZA KIBAILOJIA NA SUMU
PAMOJA NA UANGAMIZAJI WAKE**

**[(Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) na Nyongeza ya Nane, Kanuni ya
7(1)(b) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016)]**

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
DODOMA

Novemba, 2018.

HOTUBA YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU AZIMIO LA KURIDHIA MKATABA WA KIMATAIFA WA KUZUIA UENDELEZAJI, UZALISHAJI, ULIMBIKIZAJI WA SILAHA ZA KIBAILOJIA NA SUMU PAMOJA NA UANGAMIZAJI WAKE; (The Convention on Prohibition of Development, Production and Stockpiling of Bacteriological (biological) and Toxin Weapons and their Destruction BTWC)

(Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) na Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 7(1)
(b) ya Kanuni za Bunge la Toleo la Januari, 2016)

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa ni miongoni mwa nchi ambazo zimesaini na kuridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa. Mikataba hii ni pamoja na ile inayolinda haki za binadamu, utawala bora, masuala ya kidemokrasia, mazingira n.k. Pamoja na hayo Tanzania imekuwa ikiunga mkono juhudhi mbalimbali zinazofanywa duniani kuhakikisha kuwa kila raia anaishi kwa amani na usalama.

Mheshimiwa Spika, hapa karibuni jitihada hizi zimeanza kuingia dosari kubwa. Ni matumaini ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa mikataba kama hii inayolenga usalama wa raia, haki za kuishi na masuala yote ya amani itaheshimiwa.

2. MAUDHUI YA AZIMIO LA MKATABA HUU

Mheshimiwa Spika, azimio hili limekuja wakati muafaka ambapo baadhi ya nchi duniani zinakabiliwa na matatizo mengi ya kiusalama yanayotokana na kusambaa kwa magonjwa yanayotengenezwa kimkakati na vifo kwa kutumia bakteria, virusi hatarishi kwa binadamu, wanyama, mimea na mazingira pamoja na sumu.

Mheshimiwa Spika, kuna aina nyingi za bakteria, sumu au virusi ambavyo vinaweza kutegenezwa kwa kutumia vifaa vyta kimaabara ambavyo kimsingi vinaweza kuleta madhara makubwa kwenye jamii. Silaha hizi za kibailojia zinaweza kusababisha vifo vyta mamilioni ya watu ndani ya muda mfupi sana kutokana na uwezo wake wa kuharibu mishipa ya damu, moyo, neva za fahamu, kushambulia mifumo ya upumuaji n.k. Vilevile, silaha zile zenye vimelea vyta sumu na huweza kuwekwa ardhi kwa muda wa miaka mingi na hivyo kuhatarisha maisha viumbhai wa eneo hilo kila wanapozaliwa.

Mheshimiwa Spika, silaha hizi za sumu za kibailojia husafirishwa kwa njia rahisi japokuwa ni silaha zinazohitaji uangalifu mkubwa kwani madhara yake ni makubwa sana, baadhi yake ni mfano wa anthrax au kimeta na kuharibika kwa urahisi (quick decay). Kutokana na utengenezaji wa silaha hizi za kibailojia ni vyema ikafahamika kuwa kiasi kidogo cha sumu hizi kinaweza kusababisha pia magonjwa ya mlipuko na ya kuambukiza endapo uhifadhi wake haukuwa mzuri. Ipo mijadala mikubwa inayoendelea duniani kuhusu baadhi ya

magonjwa yanayoua sana kama ebola, ukimwi ikilenga kutafuta ukweli iwapo magonjwa haya yametengenezwa na aina fulani za bakteria au virusi ambavyo ni moja ya silaha za kibailojia.

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa vimelea vya sumu hizi za kibailojia zinaweza kuwekwa katika vyanzo vya maji, wanyama waliopeba vimelea wa bakteria au virusi, mizoga ya wanyama , hewa, mimea, n.k Mfano, Mwaka 1940, nchi ya Japan ilipeleka mchele wa msaada na ngano zilizochanganyika na vimelea vya ugonjwa wa tauni nchini China na Manchuria ambapo maelfu ya wananchi walidhurika. Vilevile, katika tafiti ya kutengeneza silaha hizi za Kibailojia nchini Japan mwaka 1937 wafungwa zaidi ya 10,000 walifariki kwa kujaribiwa kuwekewa vimelea hatari vyenye sumu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tutakumbuka sakata la ugonjwa wa kimeta (anthrax) duniani ambapo vimelea vya bakteria waletao mathara kwenye mapafu hususani kwa mifugo vilisambazwa kwa njia ya unga/poda kwa kutumia njia za usambazaji wa barua na hivyo maelfu ya binadamu waliathirika na vimelea vya ugonjwa huu. Mwaka 2001, Shirika la Upelezi la Marekani (FBI)lilibaini aina hiyo ya bakteria katika mji wa New Jersey. Hii ni baadhi tu ya mifano ya matukio hatari ambayo yanaweza kusababishwa na silaha za kibailojia.

Mheshimiwa Spika, hii ina maana kwamba kuendelea kukua kwa teknolojia, muingiliano wa watu duniani ambayo huhatarisha pia

usalama wa mipaka ya nchi, kuibuka kwa vikundi mbalimbali vya uhalifu na ugaidi, chokochoko baina ya nchi nanchi, vinaweza kuwa kati ya vichocheo muhimu vya utengenezaji wa silaha hizi za kibaolojia au silaha za sumu.

Mheshimiwa Spika, pamekuwa na taarifa mbalimbali ambazo zinatoa tuhuma kwa mataifa makubwa duniani kuwa shehemu ya utengenezaji wa silaha hizi za kibailojia hususani zile zenyen teknolojia kubwa za kimaabara na za utengenezaji wa madawa.Taarifa hizi zinatoa angalizo kwa mataifa mengine kuchukua hatua za kukabiliana na jambo hili ambalo tayari linaleta tishio kubwa kwa usalama wa dunia.

Mheshimiwa Spika, katika nchi zetu hizi changa kiuchumi na teknolojia si rahisi sana silaha hizi kutengenezwa japo ni rahisi sana kwa silaha hizi kuingizwa na kutumiwa vibaya kwa kutumia watu au vikundi mbalimbali vinavyohatarisha usalama.

Mheshimiwa Spika, serikali ya Tanzania ilisaini mkataba huu tangu tarehe 10 April, 1972 lakini haukuridhiwa. Kwa hiyo kuridhiwa kwa mkataba huu ni fursa kwa nchi yetu kujadili, kupata wataalamu mbalimbali duniani ambao wanajua kwa undani masuala haya ya silaha za kibaolojia, na hata kupata wataalamu wa kuja kufundisha wataalamu wetu kuhusiana na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo kuridhiwa kwa mkataba huu kunatoa tahadhari na fursa zaidi kwa serikali kuhakikisha inaandaa na kuboresha mifumo yake ya kiulinzi na endapo kunaripotiwa silaha za aina hii au kumetokea madhara yanayosababishwa na aina yoyote ya silaha za kibailojia basi mifumo hiyo iwe imara kukabiliana na janga lolote la aina hiyo(detention systems).

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 1(2) ya azimio hili inazitaka nchi wanachama kujizua kwa **namna yoyote ile kujihusisha** na uendelezaji,uzalishaji,ulimbikizaji au kujipatia au kuhifadhi silaha, vifaa au namna ambayo inaweza kutumika katika matumizi yoyote ya hatari au katika matumizi ya silaha.

Mheshimiwa Spika, azimio hili linakataza **matumizi yoyote ya silaha** za kibailojia pasipo kuainisha matumizi yapi yanaruhusiwa na yapi hayaruhusiwi au sio sahihi, tofauti na taarifa iliyowasilishwa kwenye kamati kuhusu azimio hili katika ukurasa wa 5 sehemu ya 4 kifungu kidogo cha pili ambacho kinaelezea faida ya kuridhia mkataba huu. Sehemu hii inasema “**kuwa sehemu ya uhamasishaji wa matumizi sahihi na salama ya silaha za kibailojia na sumu. Aidha nchi yetu itaweza kubadilishana vifaa,teknolojia, malighafi zinazotumika katika utengenezaji wa silaha za kibailojia na sumu kwa minajili ya kiusalama**”. Hili linabidi liangaliwe kwa umakini ili kuondoa mashaka au jambo lolote linaloweza kuja kuigharimu nchi yetu huko baadae endapo itagundulika kwa namna yoyote inazalisha, inaendeleza, inalimbikiza au kujipatia silaha za namna hii.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo iwapo nchi yoyote ina silaha za namna hiyo inapaswa kuziangamiza au kuzibadilishia matumizi mapema iwezekanavyo ndani ya muda wa miezi tisa baada ya kuanza kutumika kwa mkataba huu na si vinginevyo. Hivyo basi, serikali iweke wazi adhma yake ya kutaka fursa ya kubadilishana vifaa, teknolojia na malighafi zinazotumika katika utengenezaji wa silaha hizi za kibailojia kama ilivyoelezwa katika ripoti iliyotolewa kwa wajumbe wa kamati.

3. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, pamoja na nchi yetu kuridhia mikataba mbalimbali bado imekuwa nyuma katika kutunga sheria ambazo zinasimamia mikataba hii. Mara nyingi nchi yetu huishia katika hatua ya pili ya utekelezaji wa mikataba hii ambapo hatua ya kwanza ni kuweka saini (signing), kuridhia (ratification) na tatu ni utekelezaji wa sheria kwa kutunga sheria za ndani (domestication) .Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inategemea kuona serikali ikitunga sheria itakayolinda utekelezaji wa mkataba huu.

Naomba kuwasilisha,

.....
MASOUD A. SALIM(MB)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI-WIZARA YA ULINZI NA
JESHI LAKUJENGA TAIFA**

14.11.2018